

## **Kitabu cha kwanza cha Mambo ya Nyakati**

### **MAZINGIRA YA 1 NA 2 MAMBO YA NYAKATI**

Kama ilivyokuwa vitabu vya Samweli na Wafalme, Mambo ya Nyakati ni vitabu viwili katika Biblia zetu, lakini katika Biblia ya Kiebrania ni kitabu kimoja tu. Mwandishi hakutaja jina lake, ingawa alitaja majina ya baadhi ya vitabu na maandiko mengine alipopata habari zake (1 Nya 9:1; 27:24; 29:29; 2 Nya 9:29; 16:11; 24:27; 33:19; 35:25).

Katika Mambo ya Nyakati tunapata masimulizi ya matukio yaliyotokea Israeli wakati wa vitabu vya Samweli na Wafalme. Lakini vitabu hivyo vinatofautiana na vile vya Samweli na Wafalme katika mtindo wa uandishi na mambo yaliyomo. Mwandishi wa Mambo ya Nyakati aliandika kwa ajili ya watu wa wakati maalumu akiwa na makusudi yake ya kipekee.

#### **Hali ya wakati ule**

Kitabu cha Mambo ya Nyakati kiliandikwa miaka mingi baada ya Israeli na Yuda kupelekwa kifungoni. Watu wengi wa ufalme wa kaskazini waliopolekwa sehemu mbalimbali za ufalme wa Uashuru miaka ya 732 na 722 k.K., walitawanyika miongoni mwa watu wa sehemu zile, na kwa jumla walipototeza ufahamu wa taifa lao. Watu wa ufalme wa kusini waliopolekwa kifungoni Babeli katika awamu mbalimbali kati ya 605 na 582 k.K., kwa jumla walikumbuka ukabila wao. Waajemi waliposhinda na kuteka Babeli mwaka wa 539 k.K., waliwapa Wayahudi ruhusa karudi katika nchi yao. Waliorudi walikuwa baadhi ya wale wa kundi hilo la pili. Wengine walirudi baadaye.

Watu wengi zaidi wa wale waliorudi hawakuona nchi ya Palestina hapo awali, na bila shaka walijua kidogo sana kuhusu hekalu na ibada yake. Hao walikuwa watu ambao mwandishi wa Mambo ya Nyakati aliwaandikia. Alitaka kuwapa ujuzi wa mazingira ya nchi na dini yao. Zaidi ya hayo, alitaka waelewe kwamba walikuwa zaidi kuliko kikundi cha watu waliohamia ili waishi katika nchi ya mababu zao. Kwa watu hao, taifa lililokuwepo kabla ya kifungo liliendelea, na maisha yao yalijengwa juu ya msingi wa ufalme wa Daudi na ukuhani wa Kilawi.

#### **Alama kubwa za Mambo ya Nyakati**

Mungu alikuwa na makusudi yake alipotaka kuwaimarisha watu wake katika nchi yao tena. Alikuwa bado anatawala mambo ya historia yao, na ahadi zake alizowapa Daudi na watu wa nasaba yake zilihitiwa kutimizwa. Kwa hiyo mwandishi wa Mambo ya Nyakati alichagua na kupanga masimulizi yake kwa uangalifu, ili wasomaji wake waweze kuona umuhimu wa kujengewa taifa lao upya kufuatana na makusudi ya Mungu. Ingawa alifuatia historia ya Israeli kuanzia mfalme wa kwanza, Sauli, hadi wakati wa kifungo cha Babeli, alimtaja Sauli kwa kifupi tu. Hali kadhalika alisema maneno machache tu kuhusu ufalme wa kaskazini. Alishughulika hasa na nasaba ya ufalme wa Daudi na hekalu la Yerusalemu ambalo wafalme hao walihusika nalo.

Ufalme wa kaskazini ulitokana na mifarakano na ufalme uliochaguliwa na Mungu, yaani wa Daudi, na dini yake ilikuwa ya maasi ya ibada ya kweli ya Mungu ambayo mahali pake rasmi palikuwa Yerusalemu. Mwandishi wa Mambo ya Nyakati hana nia ya kuwavutia wasomaji wake kuhusu ufalme wa kaskazini na mambo yake ya dhambi. Kwake ufalme wa Daudi ni wa pekee uliohibitishwa, na Yerusalemu ni jiji kuu la pekee lililochaguliwa. Alifanya bidii nyingi kuonyesha kutokana na historia ya ufalme wa kusini (yaani nasaba ya Daudi) jinsi dini ya pekee iliyotolewa na Mungu ilivyokuwa na maana sana katika maisha ya watu wa kweli wa Mungu.

Kutokana na lengo kuu la mwandishi, hata maelezo ya Mambo ya Nyakati yanatofautiana na maelezo ya matukio yale yale katika vitabu vya Samweli na Wafalme. Habari kama zile za dhambi ya Daudi na Bathsheba na zile zinazohusu matatizo ya nyumbani mwake hazikuandikwa. Madhumuni ya mwandishi hayakuwa kuchunguza maisha ya watu binafsi, bali kuonyesha jinsi ufalme wa Daudi ulivyoimarishwa pamoja na mpango wa dini na maisha ya kitaifa ya Israeli kuwa mambo yasiyoweza kutenganishwa. Kwa upande mwingine, mwandishi aliongeza mambo mengi yasiyoandikwa katika Samweli na Wafalme, hasa mambo yanayohusu mpango wa dini ya Israeli wakati wote wa ufalme huo.

Hamu kubwa ya mwandishi ni kwamba, watu waishio katika Israeli baada ya kifungo cha Babeli wapange maisha yao ya kitaifa juu ya msingi wa dini ya kweli. Kwa sababu hiyo Walawi ambao hawakutajwa sana katika Wafalme walitajwa mara nyingi katika Mambo ya Nyakati. Kwa mwandishi wa Mambo ya Nyakati, dini ya pekee inayofaa kuipokea ni ile iliyojengwa juu ya msingi wa kanuni za Walawi, yaani ukuhani wa Haruni na hekalu la Yerusalemu.

#### **MUHTASARI WA 1 MAMBO YA NYAKATI**

1:1-9:34                      Orodha za vizazi (nasaba) vya makabila ya Israeli  
9:35-22:1                  Utawala wa Daudi  
22:2-29:30                Maandalizi kwa hekalu